## MUUNDO WA KIKUNDI CHA…………………………



# KATIBA YA KIKUNDI

1. **SURA YA KWANZA**
   **TAARIFA ZA KIKUNDI**
   Kikundi cha **MAMA`S VISIONARY GROUP** kilianza mnamo tarehe **15** mwezi **03** mwaka **2020** kikiwa na wanachama waanzilishi **05** wote ni wanawake. Kikundi kinapatikana katika Kata ya MJIMWEMA Mtaa wa **UNGINDONI.** Kikundi hiki kinajishughulisha na **HOTEL/MGAHAWA**
   1.1 Kikundi chetu kinajulikana kwa jina la **MAMA`S VISIONARY GROUP**
   1.2 Anwani ya kikundi ni S.L.P 90384.
   1.3 Kikundi kina akaunti na ……………………….katika Benki ya ……………………

2. **SURA YA PILI**
   2.1 Lengo kuu la kikundi ni:
   **Kusaidiana Kwenye Shida na Raha**

   **2.2 Madhumuni ya kikundi**
   1. Kukuza mtaji wa biashara
   2. Kuongeza wanachama
   3. Kumiliki biashara nyingi zaidi

3. **SURA YA TATU**
   **3.1 UANACHAMA**
   Kikundi hiki kina wanachama **05** wanawake wote na kina mpango wa kupokea wanachama wapya **10** hadi kufikia 20/06/2023.

   **3.1 UTARATIBU WA KUWA MWANACHAMA**
   Muombaji anatakiwa aandike barua ya maombi ya uanachama akiambatanisha na nakala ya kitambulisho chake cha kupiga kura,cha taifa pamoja na barua kutoka kwa kiongozi wa Serikali ya mtaa wake kwa ajili ya utambulisho.

   **3.2 SIFA ZA MWANACHAMA**
   1. Awe na umri usiopungua miaka 18 na kuendelea
   2. Awe raia wa Tanzania
   3. Awe mkazi wa eneo husika
   4. Awe na akili timamu
   5. Awe mwenye kujitoa kufanya kazi wakati wowote pindi atakapohitajika na kikundi
   6. Awe mwenye kutambua wajibu wake na asiwe mwenye tamaa.

   **3.3 WAJIBU WA MWANACHAMA**
   1. Kudumisha upendo,heshima,mshikamano na amani miongoni mwa wanachama wenzake wa kikundi pamoja na jamii kwa ujumla bila ya ubaguzi wa aina yoyote
   2. Kuomba na kupata taarifa zinazohusu shughuli za kikundi
   3. Kuchangia na kutoa maoni au kupendekeza jambo lolote katika vikao au mikutano ya kikundi pale inapobidi kwa mujibu na taratibu za katiba ya kikundi
   4. Kujitolea kwa hali na mali
   5. Kutoa michango ya kila mwezi ada kwa mwezi.

CamScanner

### 3.4 HAKI ZA MWANACHAMA

1. Kuchagua na kuchaguliwa kuwa kiongozi
2. Kuorodheshwa katika daftari la kudumu la wanachama
3. Kupiga kura kwenye mkutano mkuu
4. Kupata habari, taarifa, elimu za huduma zinazotolewa na kikundi pamoja na rasilimali za kikundi.
5. Kusikilizwa,kuheshimiwa na kujitetea kwa mujibu wa kanuni na taratibu za kikundi

### 3.5 KUPOTEZA UANACHAMA

1. Kutoshiriki katika shughuli za kikundi bila taarifa muhimu
2. Kushindwa kutimiza majukumu yake kikatiba
3. Kutofuata na kutekeleza malengo, madhumuni na kazi za kikundi pamoja na kuwa na mienendo isiyokubaliki na kikundi kulingana na taratibu za kikundi
4. Kufariki dunia

## 4. SURA YA NNE

### 4.1. MUUNDO WA UONGOZI

Kutakuwa na viongozi wafuatao:

1. Mwenyekiti
2. Katibu
3. Mweka hazina

### 4.2 MAJUKUMU YA VIONGOZI

#### 1. MWENYEKITI WA KIKUNDI

a) Atakuwa ndiye kiongozi mkuu wa kikundi na atakayehakikisha kuwepo kwa utendaji wa shughuli za kikundi zinafanyika kwa mujibu wa katiba na taratibu zilizowekwa
b) Atahakikisha kunakuwepo ufanisi katika utendaji wa shughuli za kikundi
c) Ataidhinisha taarifa ya mwaka itakayowasilishwa kwenye mkutano mkuu
d) Kwa kushirikiana na katibu mkuu ataidhinisha mihutasari ya mikutano mbalimbali ya kikundi
e) Ataongoza mikutano yote ya kikatiba
f) Atasimamia na kulinda maslahi ya wanachama
g) Atahakikisha kua katiba ya kikundi inasimamiwa na kutekelezwa
h) Ataidhinisha matumizi ya fedha ya kikundi

#### 2. KATIBU MKUU

a) Atatunza kumbukumbu zote za kikundi, muhuri wa kikundi pamoja na kutunza mihutasari ya mikutano
b) Atatunza,ataandaa agenda na kusimamia, kutunza mikataba mbalimbali ya kikundi
c) Ndiye mshauri mkuu wa utendaji wa kikundi
d) Ataitisha vikao kwa kushauriana na mwenyekiti
e) Atawezesha upangaji wa shughuli,kubuni na kuratibu miradi ya kikundi
f) Atasaini hundi za kikundi

### 3. MWEKA HAZINA

a) Atatunza vitabu vya fedha na mahesabu ya kikundi
b) Atawajibika katika malipo yatakayotolewa muda wowote kwa idhini ya kikundi
c) Atakuwa mshauri mkuu katika masuala yote yanayohusiana na fedha
d) Kukusanya na kupokea mapato ya kikundi
e) Atakuwa mtia saini katika kitabu cha kuchukua fedha Benki ama kwenye taasisi yoyote ya fedha pamoja na wajumbe wawili wa kamati tendaji
f) Atatoa taarifa za mapato na matumizi katika vikao vya kikatiba

### 4.3 VIGEZO VYA KUONDOLEWA KWENYE UONGOZI

1. Kifo cha kiongozi yeyote
2. Ubadhilifu wa mali za kikundi
3. Kufungwa kifungo kinachozidi miezi sita kutokana na makosa ya jinai
4. Endapo hatowajibika katika kazi au kupungukiwa na akili

### 4.4 AWAMU ZA UONGOZI

Uchaguzi wa viongozi utafanyika kila baada ya miaka miwili. Kiongozi anaweza kuendelea na uongozi kulingana na makubaliano ya wanachama

## 5. SURA YA TANO

### 5.1 VYANZO VYA FEDHA

Kikundi kitakuwa na vyanzo vya fedha vifuatavyo :

a) Mapato yatokanayo na biashara
b) Ada ya kila mwanachama
c) Faida kutoka na mkopo wa mwanachama

### 5.2 SHUGHULI ZA KIKUNDI NI:-

1. Kukodisha sahani za kulia chakula.
2. Kukodisha viti.
3. Kukodisha masufuria.
4. Mgahawa mama lishe kenye kutoa huduma ya chai na vitafunwa kwa asubui na kwa mchana chakula.

### 5.3 UTARATIBU WA KUGAWANA FAIDA

Utaratibu wa kugawana fedha kwa wanachama ni kila mwisho wa mwaka inayotokana na faida inayopatikana kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya kikundi

Faida hiyo itakuwa na mgawanyo kama ifuatavyo:-

- Itagawanywa kwa kila mwanachama ambayo itatoka kwenye mfuko

## 5. SURA YA SITA

### 6.1 MIKUTANO/ VIKAO VYA KIKUNDI

Kutakuwa na vikao vitatu vya kikundi
Kikao cha kila mwezi
Vikao vya dharura
Kikao cha mwaka

### 6.2 KIKAO CHA MWEZI

a. Ni kwa ajili ya kujadili na kupitia taratibu za ufanyaji kazi kwa mwezi

b. Ndio unaopokea taarifa ya mapato na matumizi ya kikundi na kutolea marekebisho

### 6.3 KIKAO CHA DHARURA

Ni kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayojitokeza kwa dharura katika kikundi

### 6.4 KIKAO CHA MWAKA / MKUTANO MKUU

1. Ni kwa ajili ya kujadili na kupitia mafanikio na changamoto mbalimbali za kikundi
2. Ndio mkutano mkuu wenye mamlaka ya mwisho ya kikundi
3. Ndio unaopokea taarifa ya kikundi na kutoa maamuzi
4. Ndio utakaokuwa na uwezo wa kumsimamisha kiongozi au mwanachama asiyefuata taratibu za kikundi

5 Kupitia mpango kazi wa kikundi wa mwaka

### 6.5 MAREKEBISHO YA KATIBA

Marekebisho ya katiba yatafanyika kwa maandishi na yatajadiliwa na kamati tendaji na mwisho Mkutano mkuu.
Kwenye mkutano mkuu wakikubaliana kufanya marekebisho itatakiwa kupigiwa kura ya ndio kwa asilimia sabini na tano (75%) ya wanakikundi.

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KIKUNDI CHA MAMA`S VISIONARY GROUP WA KUPITISHA KATIBA NA KUSAJILI KIKUNDI KILICHOFANYIKA TAREHE 25/01/2023 UNGINDONI

MAHUDHURIO

| S/N | JINA | WADHIFA | SAINI |
|---|---|---|---|
| 1. | NINA J. KALLUVYA | MWENYEKITI | |
| 2. | SALOME LEONARD KIALUZI | KATIBU | |
| 3. | GODLIVER C. MWAMPAMBA | M/ HAZINA | |
| 4. | SHAMIRA ISSA TINNA | MJUMBE | |
| 5. | AMINA YUSUPH JULIUS | MJUMBE | Ayusuph |

**AGENDA ZA KIKAO**

1. Kufungua Kikao
2. Kupitisha katiba
3. Kusajili kikundi
4. Kufungua akaunti
5. Kufunga Kikao

**AGENDA NA 1. KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 10:00 alasiri kwa aliwakaribisha wajumbe na kuwaeleza wajumbe kuwa tutakua na agenda zipi kwa siku hiyo na kutupongeza kwa umoja wetu tuliouonyesha tena kama wanakikundi kumaliza mwaka mwingine pamoja.

**AGENDA NA 2. KUPITISHA KATIBA**

Mwenyikiti aliwasomea wajumbe katiba ya kikundi na wajumbe waliielewa na wote kwa pamoja walikubalina kwamba katiba ipitishwe.

**AGENDA 3. KUSAJILI KIKUNDI**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe juu ya umuhimu wa kusajili kikundi, wajumbe waliafiki na kukubaliana kwa pamoja tuanze taratibu za kusajili kikundi, viongozi watatu ambao ni mwenyekiti, katibu, na mweka hazina na watashughulikia usajili.

**AGENDA 4 KUFUNGUA AKAUNTI**

Mwenyekiti alitoa taarifa kua baada ya kufanikiwa kusajili kikundi tutaanza na ufatiliaji wa akaunt ya bank.

**AGENDA NA 5 KUFUNGA KIKAO**

Kikao kilifungwa mnamo saa 11:30 jioni kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao.

.............................
KATIBU

.............................
MWENYEKITI

CamScanner

# KIKUNDI CHA MAMA`S VISIONARY



## WASIFU WA MWENYEKITI

| | |
|---|---|
| JINA | : NINA J. KALLUVYA |
| TAREHE YA KUZALIWA | : 25.03.1979 |
| MAHALI | : DAR ES SALAAM |
| HALI YA NDOA | : NIMEOLEWA |
| URAIA | : MTANZANIA |
| NAMBA YA SIMU | : 0652 579 830 |
| ELIMU | : . KIDATO CHA NNE |
| UZOEFU | : MJASILIAMALI |
| WADHIFA | : MWENYEKITI |
| SAINI | : 03/02/2023 |

CS CamScanner



# KIKUNDI CHA MAMA`S VISIONARY

## WASIFU WA KATIBU

| | |
|---|---|
| JINA | : SALOME LEONARD KIALUZI |
| TAREHE YA KUZALIWA | : 07.07.1988 |
| MAHALI | : DAR ES SALAAM |
| HALI YA NDOA | : SIJAOLEWA |
| URAIA | : MTANZANIA |
| NAMBA YA SIMU | : 0716 351 261 |
| ELIMU | : DARASA LA SABA |
| UZOEFU | : MJASILIAMALI |
| WADHIFA | : KATIBU. |
| TAREHE | : 03/02/2023 |

CamScanner

## KIKUNDI CHA MAMA`S VISIONARY



## WASIFU WA MWEKA HAZINA

| | |
|---|---|
| JINA | : GODLIVER C. MWAMPAMBA |
| TAREHE YA KUZALIWA | : 29.10.1998 |
| MAHALI | : DAR ES SALAAM |
| HALI YA NDOA | : SIJAOLEWA |
| URAIA | : MTANZANIA |
| NAMBA YA SIMU | : 0765 601 452 |
| ELIMU | : DARASA LA SABA |
| UZOEFU | : MJASILIAMALI |
| WADHIFA | : MWEKA HAZINA |
| TAREHE | : 03/02/2023 |

CamScanner

### 3. MWEKA HAZINA

a) Atatunza vitabu vya fedha na mahesabu ya kikundi
b) Atawajibika katika malipo yatakayotolewa muda wowote kwa idhini ya kikundi
c) Atakuwa mshauri mkuu katika masuala yote yanayohusiana na fedha
d) Kukusanya na kupokea mapato ya kikundi
e) Atakuwa mtia saini katika kitabu cha kuchukua fedha Benki ama kwenye taasisi yoyote ya fedha pamoja na wajumbe wawili wa kamati tendaji
f) Atatoa taarifa za mapato na matumizi katika vikao vya kikatiba

### 4.3 VIGEZO VYA KUONDOLEWA KWENYE UONGOZI

1. Kifo cha kiongozi yeyote
2. Ubadhilifu wa mali za kikundi
3. Kufungwa kifungo kinachozidi miezi sita kutokana na makosa ya jinai
4. Endapo hatowajibika katika kazi au kupungukiwa na akili

### 4.4 AWAMU ZA UONGOZI

Uchaguzi wa viongozi utafanyika kila baada ya miaka miwili. Kiongozi anaweza kuendelea na uongozi kulingana na makubaliano ya wanachama

## 5. SURA YA TANO

### 5.1 VYANZO VYA FEDHA

Kikundi kitakuwa na vyanzo vya fedha vifuatavyo :

a) Mapato yatokanayo na biashara
b) Ada ya kila mwanachama
c) Faida kutoka na mkopo wa mwanachama

### 5.2 SHUGHULI ZA KIKUNDI NI:-

1. Kukodisha sahani za kulia chakula.
2. Kukodisha viti.
3. Kukodisha masufuria.
4. Kamgahawa ka mama lishe kenye kutoa huduma ya chai na vitafunwa kwa asubui na kwa mchana chakula.

### 5.3 UTARATIBU WA KUGAWANA FAIDA

Utaratibu wa kugawana fedha kwa wanachama ni kila mwisho wa mwaka inayotokana na faida inayopatikana kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya kikundi

Faida hiyo itakuwa na mgawanyo kama ifuatavyo:-

- Itagawanywa kwa kila mwanachama ambayo itatoka kwenye mfuko

MAMA`S VISIONARY GROUP
S.L.P 90384,
KIGAMBONI,
**25/01/2023.**

MKURUGENZI,
MANISPAA YA KIGAMBONI,
S.L.P 36009,
**DAR ES SALAAM.**

**K.K**
AFISA UMAENDELEO YA JAMII,
MANISPAA YA KIGAMBONI,
S.L.P 36009,
**DAR ES SALAAM.**

**K.K**
MTENDAJI WA KATA,
KATA YA MJIMWEMA,
**KIGAMBONI.**

K.K
MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA,
MTAA UNGINDONI, MTENDAJI WA MTAA
**KIGAMBONI.** MTAA WA UNGINDONI

**YAH: MAOMBI YA KUSAJILI KIKUNDI.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Sisi wanakikundi cha **MAMA`S VISIONARY** kilichopo Mtaa wa **Ungindoni** Kata **Mjimwema** Wilaya ya **Kigamboni.**

Tunaomba kusajili kikundi chetu ili tuweze kutambulika kisheria na kupata furasa mbalimbali za kijamii.

Tunaimani ya maombi yetu yatapewa uzito unaostahili.

Asante

…………………………..
**Katibu**

CamScanner

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**
**MJIMWEMA- KATA YA MJIMWEMA**
**S.L.P 36009 KIGAMBONI, DAR ES SALAAM**

OFISI YA SERIKALI YA MTAA
MTAA UNGINDONI,
S.L.P 36009,
TAREHE ..06/02/2023..........

**Kumb. Na**......6/2023/......................

MKURUGENZI,
MANISPAA YA KIGAMBONI,
S.L.P 36009,
DARE S SALAAM.

**YAH: UTAMBULISHO WA KIKUNDI CHA** ......MAMA'S VISIONARY
......GROUP..........................

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Nakitambulisha kikundi cha ......MAMA'S VISIONARY GROUP... kuwa ni kikundi cha ......WANAWAKE WAJASIRIAMALI...... kilichopo katika mtaa wa ......UNGINDONI..........

Kinajishughulisha na
......MAMA LISHE-..........................
..................................................

Aidha wajumbe wake wote ni wakazi wa
......UNGINDONI..........

Naomba wasajiliwe.

Wako

..................................
**SAID MOHAMED KISANDUKU**
**MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA**
**MJIMWEMA**

MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA UNGINDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI**
**[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kigamboni]**

Simu: +255 22-2928468
Fax: +255 22-2928469
Barua pepe: info@kigamboni.go.tz
Tovuti: www.kigambonimc.go.tz

S.L.P. 90384,
KIGAMBONI,
DAR ES SALAAM,

**TANZANIA.**

Tarehe: 25/01/2025

## MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI

Kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Sisi MAMA's VISIONARY GROUP S.L.P 90384 Dar Es Salaam Mahali yalipo Makao Makuu ya Kikundi **Ungindoni Mjimwema.**

Tunawasilisha maombi ya usajili wa Kikundi cha MAMA's VISIONARY GROUP Kitafanya kazi katika Kata ya Mjimwema Mtaa wa Ungindoni Wilaya ya Kigamboni Shughuli ya kikundi ni Catering/Mgahawa

Tunaambatanisha nakala za;

a) Majina ya wanachama waanzilishi na saini zao
b) Katiba ya kikundi
c) Maelezo binafsi ya viongozi wa kikundi
d) Wasifu wa Viongozi(Mwenyekiti,Katibu na Mweka Hazina)
e) Muhtasari wa kikao cha kikundi kupitisha katiba
f) Barua ya maombi ya usajili wa Kikundi kwa Mkurugenzi wa Manipaa (K/K Afisa Maendeleo ya Jamii,Afisa mtendaji wa Kata na Mtaa)
g) Kiambatasho cha umri kwa vikundi vya Vijana(Nida,Leseni ya Udereva Cheti cha kuzaliwa).

Uthibitisho wa kikundi/Mwenyekiti/Katibu/M/Hazina wa kikundi

Jina: NINA J KALUWA wadhifa MWENYEKITI saini NKat.

Jina: Solomon Lunabi wadhifa KATIBU saini So

Jina: GODLIVER MWANAMBOT wadhifa M/HAZINA saini GChwa

**Uthibitisho wa viongozi wa serikali za Mitaa na Kata wa mahali ambapo kikundi hiki kinafanya shughuli zao**

**Afisa Mtendaji wa Kata**

Jina

Sahihi ..

**Afisa Mtendaji wa Mtaa**

Jina NAIMA OKIDA

Sahihi 11/2/2023.

AFISA MTENDAJI MTAA UNGINDOI

Nathibitisha uwepo wa kikundi hiki na wanafanya shughuli zao.

**Afisa Maendeleo ya Jamii**

Jina

Sahihi

**AZIMIO LA KUANZISHA KIKUNDI KIJAMII/KIUCHUMI CHA** MAMA'S VISIONARY GROUP

Sisi tulioweka saini kwenye kikao kilichofanyika tarehe 25/01/2023, katika Mtaa wa MJIMWEMA, Kata ya UNGINDONI, tumekubaliana na kuamua kuanzisha kikundi cha **kijamii/kiuchumi kinachojulikana kwa jina la** MAMAS VISIONARY GROUP

| JINA | SAINI |
|---|---|
| 1. NINA JOHN KALWOYA | [signature] |
| 2. Salome Kinabi Kiafuu | [signature] |
| 3. Shamila Issa Tinna | [signature] |
| 4. GODLVER CHALES WAMBAMBA | [signature] |
| 5. AMINA YUSUPH JULIUS | AYusuph |

### 3. MWEKA HAZINA

a) Atatunza vitabu vya fedha na mahesabu ya kikundi
b) Atawajibika katika malipo yatakayotolewa muda wowote kwa idhini ya kikundi
c) Atakuwa mshauri mkuu katika masuala yote yanayohusiana na fedha
d) Kukusanya na kupokea mapato ya kikundi
e) Atakuwa mtia saini katika kitabu cha kuchukua fedha Benki ama kwenye taasisi yoyote ya fedha pamoja na wajumbe wawili wa kamati tendaji
f) Atatoa taarifa za mapato na matumizi katika vikao vya kikatiba

### 4.3 VIGEZO VYA KUONDOLEWA KWENYE UONGOZI

1. Kifo cha kiongozi yeyote
2. Ubadhilifu wa mali za kikundi
3. Kufungwa kifungo kinachozidi miezi sita kutokana na makosa ya jinai
4. Endapo hatowajibika katika kazi au kupungukiwa na akili

### 4.4 AWAMU ZA UONGOZI

Uchaguzi wa viongozi utafanyika kila baada ya miaka miwili. Kiongozi anaweza kuendelea na uongozi kulingana na makubaliano ya wanachama

## 5. SURA YA TANO

### 5.1 VYANZO VYA FEDHA

Kikundi kitakuwa na vyanzo vya fedha vifuatavyo :

a) Mapato yatokanayo na biashara
b) Ada ya kila mwanachama
c) Faida kutoka na mkopo wa mwanachama

### 5.2 SHUGHULI ZA KIKUNDI NI:-

1. Kukodisha sahani za kulia chakula.
2. Kukodisha viti.
3. Kukodisha masufuria.
4. Kamgahawa ka mama lishe kenye kutoa huduma ya chai na vitafunwa kwa asubui na kwa mchana chakula.

### 5.3 UTARATIBU WA KUGAWANA FAIDA

Utaratibu wa kugawana fedha kwa wanachama ni kila mwisho wa mwaka inayotokana na faida inayopatikana kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya kikundi

Faida hiyo itakuwa na mgawanyo kama ifuatavyo:-

- Itagawanywa kwa kila mwanachama ambayo itatoka kwenye mfuko